

**MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA  
WA HAKI ZA WAKULIMA WADOGO  
NA WATU WENGINE WANAOFANYA KAZI  
VIJIJINI**





# Yaliyomo

## Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wakulima Wadogo na Watu Wengine Wanaofanya Kazi Vijijini

Utangulizi .....	3
Dibaji.....	7
Ibara ya 2.....	12
Ibara ya 3.....	13
Ibara ya 4.....	14
Ibara ya 5.....	14
Ibara ya 6.....	15
Ibara ya 7.....	15
Ibara ya 8.....	15
Ibara ya 9.....	16
Ibara ya 10.....	16
Ibara ya 11.....	16
Ibara ya 12.....	17
Ibara ya 13.....	17
Ibara ya 14.....	18
Ibara ya 15.....	19
Ibara ya 16.....	20
Ibara ya 17.....	21
Ibara ya 18.....	22
Ibara ya 19.....	22
Ibara ya 20.....	23
Ibara ya 21.....	23
Ibara ya 22.....	24
Ibara ya 23.....	25

## Table of Content

---

Ibara ya 24.....	25
Ibara ya 25.....	25
Ibara ya 26.....	26
Ibara ya 27.....	26
Ibara ya 28.....	26

## **Utangulizi**

### **Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wakulima Wadogo: Historia, Ushindi na Changamoto Zijazo**

## **Kwa Ardhi yenye Haki!**

Mnamo tarehe 17 Desemba 2018, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa uliasili rasmi Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wakulima Wadogo na Watu Wengine Wanaofanya Kazi Vijijini (UNDROP). Nyenzo hii ya kisiasa tunaihesabu leo kama ushindi wa shughuli za La Via Campesina (LVC) katika muktadha wa mashambulizi ya Uliberali Mambo-leo ambayo yalitishia uwepo wa wakulima wadogo na uhuru wa chakula.

Kwa miaka mingi, vuguvugu hili (yaani LVC) lilijadiliana miongoni mwa wadau wake juu wa pendekezo la kuwa na Mkataba wa Kimataifa na mwaka 2001 wanachama wa vuguvugu la wakulima wadogo (LVC) walijadiliana kwa kina katika Kongamano la Mageuzi ya Kilimo na Haki za Wakulima Wadogo, lililoandaliwa na shirika la Serikat Pekani Indonesia (SPI), nchini Indonesia.

Baadae, 2004, wakati wa Kongamano la 4 la Kimataifa la LVC jijini Sao Paulo, vuguvugu la wakulima wadogo ulimwenguni lilipitisha Mpango Kazi wake wa kutengeneza mkataba wa kimataifa wa haki za wakulima wadogo. Mbele zaidi, katika Kongamano la Kimataifa la Haki za Wakulima Wadogo lililoandaliwa na LVC jijini Jakarta, rasimu ya kwanza ya Mkataba wa Haki za Wakulima Wadogo – Wanawake na Wanaume ilitengenezwa, ambayo ilithibitishwa na Kongamano la 5 la Kimataifa la La Via Campesina jijini Maputo, mwaka huo huo. Ndipo hapo ambapo La Via Campesina, kwa kushirikiana na wadau wengine wengi waliojiunga na mchakato, kama CETIM na FIAN International, ilianza mchakato ambao ulimaanisha miaka 18 ya maandamano ya pamoja na kuhamasishana kwa ajili ya kuunganisha, nyuzi kwa nyuzi, mkataba rasmi wa kimataifa wa kuhamasisha haki za binadamu za wakulima wadogo waume kwa wake.

Kwa mamilioni ya wakulima wadogo na wanajamii wengine wa vijijini, ambao maisha na namna ya kujikimu kwao inategemea ardhi, misitu, mito na bahari, Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa ni nyenzo ya kimkakati ya kuunganisha mavuguvugu na mapendekezo ya taasisi za vijijini. Pia inatengeneza msingi wa kisheria na msimamo wake kimataifa kuongoza sheria na sera za jamii katika ngazi zote za kitaasisi ili kuwanufaisha wale wanaoilisha dunia nzima.

Hivi sasa, wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi

---

maeneo ya vijijini wanaathiriwa na mifumo mbalimbali yenye ubaguzi pale wanapojaribu kujipatia maisha yenye staha kama wazalishaji chakula katika jamii zao. Aghalabu hukumbana na ghasia za uhamisho wa nguvu, unyanyapaa na hata vifo.

Janga la chakula lililoshamiri zaidi katika miaka ya 90 na kuendelea mpaka leo, janga ambalo limetambulika hata na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO), lilipelekea Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa kufanya utafiti, uliodhihirisha kwamba ubaguzi unaowakabili wakulima wadogo na wafanyakazi wengine vijijini una mizizi katika kukosekana kwa uwiano katika upatikanaji na udhibiti wa ardhi, baioanuwai na mali nyingine za asili. Kwa kuzuiwa kuyafikia masoko na nyenzo za uzalishaji kumezizuia jamii za wazalishaji wadogo kujipatia namna ya kujikimu.

Utafiti ulieleza kuwa udhalimu huu ulizidishwa na sera za mataifa za kilimo zilizotungwa kwa manufaa ya kundi dogo la wakulima wenye uwezo, wamiliki wa mashamba makubwa, mawakala wa viwanda vya kilimo na makampuni ya kilimo biashara. Utafiti huu ulifanywa na Kamati ya Ushauri ya UNHRC na kuasiliwa katika kikao cha 21 mwaka 2012.

Baadae, Septemba 2012, kiliundwa kikundi kazi huru baina ya mataifa (OEWIG), kilichogatuliwa mamlaka ya kujadili, kukamilisha na kisha kukabidhi kwa Tume ya Haki za Binadamu rasimu ya “Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wakulima Wadogo na Watu Wengine Wanaofanyakazi Vijijini”. Vikao vitano vya majadiliano vilifanyika kati ya 2013 na 2018. Septemba 28, 2018, katika kikao cha 39 cha Tume ya Haki za Binadamu, nchi 47 zilipiga kura kwa wingi kuunga mkono kutambulika kwa Mkataba huo wa Umoja wa Mataifa, hali iliyopelekea kuasiliwa rasmi katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa mnamo Desemba 17, 2018.

Ushindi huu wa kihistoria umekuja katika wakati muhimu, kwa kuwa leo hii zaidi ya wakulima wadogo bilioni 1.2 na familia zao, wanaounda theluthi ya idadi ya watu wote duniani, wanakumbana na ukiukwaji usiopimika wa haki zao. Hiki ni kipindi cha mmomonyoko mkubwa wa haki za wafanyakazi, wa ubinafsishaji na uharibifu wa tija itolewayo na mazingira asili; kipindi ambacho mtaji unapora sivyo kihalali ardhi, maji, madini, mafuta, mbegu na baioanuwai. Na ni kielelezo kwamba kilimobiashara, maji biashara na madini vinaongeza tu unyonyaji wa mali asili.

Leo hii wakulima wadogo wanakabiliiana na sera za serikali zisizo rafiki katika masuala ya uzalishaji na kibiashara; wanakabiliwa na mazingira mabaya ya kazi, kuondolewa kwenye ardhi na maeneo yao, na mara nyingi wanakuwa wahanga wa vitendo vya kihalifu na mauaji.

---

Wakulima wadogo ndio ambao pia mara nyingi wanakabiliwa zaidi na umaskini na njaa. Kwa mujibu wa ripoti ya 2018 ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) kuhusiana na usalama wa chakula na lishe duniani, janga la njaa linazidi kushamiri na linaathiri zaidi ya watu milioni 821, wengi wakiwa ni wakulima wadogo. Baioanuwai, ambayo wakulima wadogo hutegemea kama namna ya kujikimu ili kujenga mifumo endelevu ya chakula, inapungua, kama ilivyoelezwa katika ripoti ya FAO iliyochapishwa karibuni, 2019, “Hali ya Baioanuwai Duniani kwa Chakula na Kilimo”.

Msingi wa Mkataba huu (UNDROP) unajielekeza katika haki katika ardhi, mbegu na baioanuwai, pamoja na haki nyingine za pamoja zinazo fungamana katika uhuru wa chakula (ambao ni haki ya watu kuamua chakula chao na mifumo yao ya kilimo na haki ya kupata vyakulavyenye afya na vilivyo vya asili).

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wakulima Wadogo unachochea vuguvugu la kijamii la kuondokana na masuala na madhaifu wa sheria yanayoweza unyonyaji, ukandamizaji na uhamishaji wa wakulima wadogo kwa manufaa ya wenye mitaji kwa msaada mara nyingi wa serikali na taasisi za kimataifa. Zaidi, inatoa nyenzo ya wakulima wadogo na wafanyakazi wa vijijini kutaka serikali zao kutunga sera za umma zinazolenga kuzuia na kushughulika na udhalimu wa kijamii.

Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa pia unatambua haki ya pamoja ya wakulima wadogo kupigania upatikanaji, wa pamoja na wa mtu mmoja mmoja, wa ardhi, mbegu, maji, baioanuwai na rasilimali asili, pamoja na hifadhi jamii, huduma nzuri za afya na mazingira mazuri ya kazi. Kusisitiza kwamba haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kimazingira na za pamoja zinahusiana na hazigawanyiki, Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa unafanya kazi kama kichocheo cha mageuzi makubwa kukabiliana na vitendo haribifu vya makampuni makuu.

Kando na kuwa na ibara mahususi iliyojikita katika wajibu wake, Mkataba huu pia unatoa mlolongo wa wajibu na mapendekezo kwa nchi katika kila ibara. Hii ina maana kuwa (Mkataba) haelezei tu haki za wakulima wadogo, bali pia (unaeleza) namna na nyenzo za nchi katika kuzihakikisha haki hizo. Katika muktadha huu, Mkataba unasisitiza umuhimu na uhitaji wa mageuzi ya kilimo ilikuhakikisha haki katika ardhi.

Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa unatoa muongozo wa kidunia wa sheria na sera za mataifa zikiwa na lengo la:

- Kuboresha ulinzi wa haki za wakulima wadogo (wanaume, wanawake na vijana) na njia za kujikimu vijijini;
- Kuimarisha suala la uhuru wa chakula, mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi na utunzaji wa baioanuwai;
- Kutambulisha mageuzi ya kilimo ya kweli na kulinda jamii za wakulima wadogo dhidi ya uporaji wa ardhi;
- Kuhakikisha haki za wakulima wadogo kuhifadhi, kutumia, kubadilishana na kuuza mbegu;
- Kuhakikisha bei nzuri kwa mazao ya wakulima wadogo na usawa wa mazingira ya kazi kwa wafanyakazi vijijini, pamoja na
- Kutambua haki za wakulima wadogo wanawake na vijana na kupelekea haki jamii kwa watu wa makundi yote pasipo kubaguliwa.

Hivyo, Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa unahakikisha kwamba haki za binadamu zinatumiwa kwa watu wote badala ya watu wachache. [Mkataba] Unathibitisha kushamiri kwa haki za watu wa vijijini, unatoa mamlaka kwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa na kuwakumbusha wajibu wao wa kuhamasisha ulinzi na uenezaji wa haki za wakulima wadogo na wafanyakazi wengine vijijini.

Kwa namna hii, kazi yetu kama La Via Campesina ni kuchukua nyenzo hii mikononi mwetu na kuhamasisha mashina yetu, kuratibu mafunzo ya kisiasa kuhusu Mkataba huu, kuutumia kwa utetezi wa wakulima wadogo katika taratibu za kisheria, na kuzitaka jamii kuunda mikakati ya kitaifa na kikanda inayolenga katika utekelezaji wa Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa ili nchi, katika kila ngazi zao, kutekeleza wajibu wao wa kuhakikisha heshima na haki kwa wote wanaozalisha kwa msingi wa Uhuru wa Chakula duniani kote.

**TUNALISHA WATU WETU NA**

**TUNAJENGA VUGUVUGU LA KUIBADILI DUNIA!**

**MATAIFISHA MAPAMBANO, MATAIFISHA MATUMAINI!**

**La Via Campesina**





## Mkutano Mkuu

21 Januari 2019

---

**Kikao cha sabini na tatu**

**Ajenda kipengele cha 74 (b)**

### **Azimio lililo kubaliwa na Mkutano Mkuu tarehe 17 Desemba 2018**

*[katika ripoti ya Kamati ya Tatu (A/73/589/Add.2)]*

#### **73/165. MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA WA HAKI ZA WAKULIMA WADOGO NA WATU WENGINE WANAOFANYA KAZI VIJIJINI**

Mkutano Mkuu,

Ukikaribisha majumuisho ya Tume ya Haki za Binadamu katika azimio lake 3 9/12 la 28 Septemba 2018, 1 la Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wakulima Wadogo na Watu Wengine Wanaofanya Kazi Vijijini,

1. UnaaSili Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wakulima Wadogo na Watu Wengine Wanaofanya Kazi Vijijini, kama ulivyo katika kiambata cha azimio hili;
2. Unaalika Serikali, Wakala na Mashirika ya Umoja wa Mataifa na mashirikiano baina ya serikali mbalimbali na mashirika yasiyo ya kiserikali kusambaza Mkataba huu na kueneza uelewa na uzingatiwaji wake kwa ujumla hivyo;
3. Unamuomba Katibu Mkuu kujumuisha Mkataba huu katika toleo lijalo la Haki za Binadamu: Mkusanyiko wa Mikataba ya Kimataifa.

Mkutano Jumuishi wa 55

17 Desemba 2018<sup>1</sup>

Tazama kumbukumbu rasmi za Mkutano Mkuu, Kikao cha Sabini na tatu, Nyongeza Na.53A (A/73/53Add.1), sur. II

---

<sup>1</sup> 18-22260 (S)261218240119

\*1822260\*

**Kiambata****MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA WA HAKI ZA WAKULIMA WADOGO NA WATU WENGINE WANAOFANYA KAZI VIJIJINI**

Mkutano Mkuu,

*Kurejea* misingi iliyoainishwa katika (Katiba) Mkataba (Unaosisi) wa Umoja wa Mataifa, unaotambua utu wa asili na thamani na usawa na haki zisizoweza kutengeshwa na jamii ya watu kama msingi ya uhuru, haki na amani duniani,

*Kuzingatia* misingi iliyoelezwa katika Mkataba wa Haki za Binadamu<sup>2</sup>, Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi wa Rangi<sup>3</sup>, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni<sup>4</sup>, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa<sup>5</sup>, Mkataba wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake<sup>6</sup>, Mkataba wa Haki ya Mtoto<sup>7</sup>, Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Wafanyakazi Wote Wahamiaji na Wanafamilia wao<sup>8</sup>, mikataba inayohusiana na Shirika la Kimataifa la Kazi na mikataba mengine inayofanania ambayo imeasiliwa kiulimwengu na kikanda,

*Kusisitiza tena* Mkataba kuhusiana na Haki ya Maendeleo, na kwamba haki ya maendeleo<sup>9</sup> ni haki ya binadamu isiyoweza kutenganishwa kwa msingi kwamba kila mtu na watu wote wana haki ya kushiriki, kuchangia na kufurahia maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kisiasa, ambapo haki zote za binadamu na misingi ya uhuru inaweza kufikiwa kikamilifu,

*Kusisitiza pia* kuhusu Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wenyeji,

*Kusisitiza zaidi* kwamba haki za binadamu ni jumuishii kwa watu wote, zisizogawanyika, zenye kuhusiana, zinazo tegemeana na zinazo imarishana na zinazopaswa kushughulikiwa kwa namna ya haki na usawa, kwa viwango na msisitizo sawa, na kwa kutambua kuhamasisha na kulinda kundi moja la haki hakupaswi kuziondolea serikali wajibu wa kuhamasisha na kulinda haki nyinginezo,

Kutambua mahusiano maalum na muingiliano kati ya wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini na ardhi, maji na asili ambayo wameambatana nayo na ambayo wanaitegemea kwa ustawi wao,

Kutambua michango ya kale, sasa na ijayo ya wakulima wadogo na watu wengine

- 2 Resolution 217A(III)
- 3 United Nations, Treaty Series, vol. 660, No. 9464
- 4 See Resolution 2200 A (XXI), annex
- 5 United Nations, Treaty Series, vol.1249, No. 20378
- 6 Ibid., vol.1577, No.27531
- 7 Ibid., vol. 2220, No. 39481.
- 8 Resolution 41/128, annex.
- 9 Resolution 61/295, annex.

wanaofanya kazi vijijini katika kanda zote za dunia kwa maendeleo na utunzaji na uboreshaji wa biaoanuwai, ambayo ndio inajumuisha msingi wa uzalishaji wa chakula na kilimo duniani kote, na mchango wao katika kuhakikisha haki ya utoshelevu na uhakika wa chakula, ambao ni muhimu katika kufikiwa malengo ya maendeleo yaliyoafikiwa kidunia, pamoja na Ajenda ya Maendeleo Endelevu 2030,<sup>10</sup>

Kuzingatia kuwa wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini wanaathirika zaidi na umasikini, njaa na lishe duni,

Kuzingatia kuwawakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini wanaathirika na adha zisababishwazo na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi,

Kuzingatia zaidi kwamba wakulima wadogo wanazee duniani kote na vijana wanazidi kuhamia mijini kwa wingi na wanakipa mgongo kilimo kutokana na kukosekana kwa hamasa na ugumu wa maisha vijijini, na kutambua umuhimu wa ukuzaji uchumi mseto vijijini na uundaji wa fursa zisizo za kilimo, mahususi kwa vijana wa vijijini,

Kutahadharishwa kwa ongezeko la wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini wanaohamishwa na kufukuzwa kwa nguvu kila mwaka,

Kutahadharishwa pia na matukio mengi ya kujiua kwa wakulima wadogo katika nchi nyingi,

Kusisitiza kwamba wakulima wadogo wanawake na wanawake wengine vijijini ndio wanachukua nafasi ya msingi katika ustawi wa kiuchumi wa familia zao na katika kuchangia uchumi vijijini na nchini, ikiwamo kupitia kazi zao katika sekta za kiuchumi zisizo za kifedha, lakini mara nyingi wananyimwa haki ya umiliki na ulinzi katika ardhi, usawa katika upatikanaji wa ardhi, rasilimali za uzalishaji, huduma za kifedha, taarifa, ajira au ulinzi jamii, na mara nyingi ni wahanga wa ukatili na ubaguzi unaojidhirihisha katika namna na aina mbalimbali.

Kusisitiza pia juu ya umuhimu wa kuhamasisha na kulinda haki za mtoto aliyeko vijijini, ikiwamo kupitia kuondokana na umaskini, njaa na lishe duni, kuhamasisha elimu na afya bora, (kuwalinda) ulinzi dhidi ya hatari za kemikali na taka hatarishi, na kutokomeza ajira kwa watoto, kwa kuzingatia wajibu husika wa haki za binadamu,

Kusisitiza zaidi kwamba sababu kadhaa huwawia vigumu wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini, ikiwamo wavuvi wadogo na wafanyakazi katika sekta ya uvuvi, wafugaji, wanamisitu na jamii nyinginezo, kufanya sauti zao kusikika, kulinda haki zao za binadamu na haki zao za umiliki ardhi, na kuwahakikishia matumizi endelevu ya rasilimali asili ambazo wao huzitegemea,

Kutambua kwamba upatikanaji wa ardhi, maji, mbegu na rasilimali asili nyinginezo zimeendelea kuwa changamoto kwa watu wa vijijini, na kusisitiza

umuhimu wa kukuza upatikanaji wa rasilimali za uzalishaji na uwekezaji katika maendeleo stahiki vijijini,

Kukubali kwamba wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini wanapaswa kusaidiwa katika jitihada zao za kukuza na kufanya uzalishaji katika kilimo kwa mbinu endelevu ambazo zinashabihiana na ni rafiki kwa asili, inayotambulika kama Mama Dunia katika nchi na kanda kadhaa, ikiwamo kwa kuheshimu uwezo wa kibailoia na wa asili, wa mfumo wa kiikolojia wa kukabiliana na kuzaliana kupitia mchakato na mzunguko wa asili,

Kuzingatia mazingira hatarishi na ya kinyonyaji yaliyopo katika maeneo mengi duniani ambayo wakulima wadogo wengi na watu wengine wanaofanya kazi vijijini hulazimika kufanya kazi, mara nyingi hunyimwa fursa ya kutumia haki zao za msingi kazini na hukosa pato la kujikimu na ulinzi jamii,

Kuzingatia kwamba watu, vikundi na taasisi zinazohamasisha na kulinda haki za binadamu za wale wanaofanya kazi katika ardhi na masuala ya rasilimali asili wanakumbana na hatari kubwa ya kufanyiwa vitendo mbalimbali vya vitisho na shambulio la kimiwili,

Kutambua kwamba wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini hukabiliana na changamoto mara nyingi ya kuzifikia mahakama, maafisa usalama, waendesha mashtaka na wanasheria kiasi kwamba wanashindwa kusaka fidia au ulinzi kutokana na ukatili, unyanyasaji na unyonyaji,

Kuzingatia juu ya uvumi katika mazao ya chakula, kuongezeka kwa mlundikano na mifumo ya usambazaji wa chakula isiyo na uwiano na mahusiano ya kimamlaka yasiyo na usawa katika mnyororo wa thamani, ambayo inaathiri unufaikaji wa haki za binadamu,

Kusisitiza kuwa haki ya maendeleo ni haki ya binadamu isiyo teganishwa kwa msingi kwamba kila mtu na watu wote wana haki ya kushiriki katika, kuchangia na kufurahia maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kisiasa, ambapo haki zote za msingi za binadamu zinaweza kufikiwa,

Kurejea haki ya watu kutekeleza, kwa kuzingatia vipengele husika vya Mikataba yote ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, mamlaka yote na kamili katika utajiri na rasilimali zao za asili,

Kutambua kwamba dhana ya uhuru wa chakula imekuwa ikitumika katika nchi na kanda mbalimbali kuamua haki ya kutafsiri kufafanua mifumo yao ya chakula na kilimo na haki ya kupata afya na chakula kinachozalishwa kuendana na tamaduni kupitia njia endelevu na nzuri za kiikolojia zinazoheshimu haki za binadamu,

Kutambua kuwa mtu, mwenye wajibu kwa watu wengine na kwa jamii aliyomo, anaowajibu wa kuhamasisha na kufuatilia juu ya haki zinazotambuliwa katika Mkataba huu na katika sheria za nchi yake,

Kusisitiza umuhimu wa kuheshimu tamaduni mbalimbali na wa kukuza ustahimilivu, mazungumzo na mashirikiano,

Kutambua mikataba mbalimbali na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani kuhusiana na ulinzi wa nguvu kazi na ajira zenye staha,

Kurejea pia Mkataba wa Anuwai ya Kibaiolojia<sup>11</sup> na Itifaki ya Nagoya wa Upatikanaji wa Rasilimali Jeni na Ushirikishaji wa Haki na Sawa wa Faida zitokanazo na Utekelezaji wa Mkataba wa Anuwai ya Kibaiolojia<sup>12</sup>,

Kuzingatia zaidi kazi kubwa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa na Kamati ya Dunia ya Usalama wa Chakula katika haki ya chakula, haki ya umiliki, upatikanaji wa rasilimali asili na haki nyenginezo za wakulima wadogo, hususani Mkataba wa Kimataifa wa Mazao ya Rasilimali Jeni kwa Chakula na Kilimo<sup>13</sup>, na Miongozo ya Hiari ya Shirika katika Utawala Unaowajibika na Umiliki wa Ardhi, Uvuvi na Misitu katika Muktaadha wa Usalama wa chakula wa Taifa<sup>14</sup>, Miongozo ya Hiari ya Kulinda Uvuvi Mdogo Endelevu katika Muktaadha wa Usalama wa chakula na Utokomezaji wa Umaskini na Miongozo ya Hiari ya Ufikiwaji wa Kimaendeleo wa Haki ya Utoshelevu wa Chakula katika Muktaadha wa Usalama wa chakula wa Taifa<sup>15</sup>,

Kurejea matokeo ya Kongamano la Kimataifa la Mageuzi ya Kilimo na Maendeleo Vijijini, na Mkataba wa Wakulima Wadogo ulioasiliwa papo hapo, ambapo umuhimu wa utungaji wa mikakati stahiki ya kitaifa ya mageuzi ya kilimo na maendeleo vijijini, na utangamano wake katika mikakati ya jumla ya maendeleo ya nchi, ulisisitizwa,

Kusisitiza kuwa Mkataba huu na makubaliano mengine ya kimataifa yenye tija yatasaidia kwa pamoja kwa mtizamo wa kutilia mkazo ulinzi wa haki za binadamu,

Kudhamiria kuchukua hatua mpya katika kuwajibika kwa jumuiya ya kimataifa yenye mtazamo wa kuyafikia maendeleo madhubuti katika shughuli za haki za binadamu kwa ongezeko na uendelezaji wa jitihada za mashirikiano na mshikamano wa kimataifa,

Kukubali juu ya ulazima wa kulinda haki za binadamu za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini, na kwa ufafanuzi na matumizi ya kina ya desturi na misingi ya haki za binadamu za kimataifa zilizopo katika suala hili,

Unatamka ifuatavyo:

11 United Nations, Treaty Series, vol.1760, No. 30619.

12 United Nations Environment Programme, document UNEP/CBD/COP/10/27, annex, decision X/1

13 United Nations, Treaty Series, vol.2400, No.43345

14 Food and Agriculture Organization of the United Nations, document CL 14 4/9 (C 2013/20), appendix D.

15 E/CN.4/2005/131.annex

## Ibara ya 1

1. Kwa madhumuni ya mkataba huu, Mkulima Mdogo ni mtu yeyote anayejihusisha au anajishughulisha peke yake, au kwa kushirikiana na wengine au kama jamii, katika uzalishaji mdogo katika kilimo kwa ajili ya kujikimu na/au kwa ajili ya soko, na kimsingi anaetegemea, japo sio pekee, katika nguvukazi ya familia na njia nyingine za nguvu kazi zisizokuwa za kifedha, na anaetegemea kipekee na kujiambatanisha na ardhi.
2. Mkataba huu unamuhusu mtu yeyote yule anayejihusisha na ufundi mchundo au kilimo kidogo, upandaji wa mazao, ufugaji, uvuvi, shughuli za misitu, uwindaji na ukusanyaji matunda na mizizi, na kazi za mikono zinazohusiana na kilimo au kazi nyingine vijijini. Pia unatumika kwa wanafamilia wategemezi kwa wakulima wadogo.
3. Mkataba huu pia unatumika kwa watu walio wakaazi asili na jamii za wenyeji zinazofanyakazi katika ardhi, jamii zinazohama na mifugo na watu wasio na ardhi wanaojishughulisha na shughuli tajwa hapo juu.
4. Mkataba huu pia unatumika kwa waajiriwa, kujumuisha wafanyakazi wahamiaji pasipo kuzingatia hadhi yao katika uhamiaji, na wafanyakazi wa msimu, katika mashamba, misitu na mashamba ya ufugaji wa samaki na katika biashara ya kilimo cha mazao ya viwandani.

## Ibara ya 2

1. Nchi zitaheshimu, kulinda na kutekeleza haki za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini. Zitachukua haraka hatua za kisheria, kiutawala na hatua nyingine stahiki kufanikisha kufikiwa kabisa kwa haki zilizoanishwa katika Mkataba huu ambazo upatikanaji wake hauwezi kuhakikishwa kwa sasa.
2. Msisitizo wa kipekee utaelekezwa katika utekelezaji wa Mkataba huu na katika haki na mahitaji maalum ya wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini, kujumuisha wazee, wanawake, vijana, watoto na watu wenye ulemavu, ikizingatia uhitaji wa kukabiliana na unyanyapaa na ubaguzi wa aina mbalimbali.
3. Pasipo kupuuza sheria mahususi za watu wa asili, kabla ya kuasili na kutekeleza sheria na sera, mikataba ya kimataifa na michakato mingine ya maamuzi yanayoweza kuathiri haki za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini, Nchi zitawashirikisha na kushirikiana kwa uzuri na wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini kwa kupitia vyombo vyao vya uwakilishi, kuwahusisha na kusaka kuungwa na wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini watakaoweza kuathiriwa na maamuzi kabla ya maamuzi husika kuchukuliwa, na kushughulika na michango yao, kuzingatia hali ya utofauti wa mamlaka kati ya washiriki na kuhakikisha ushiriki hai, huru, wenye tija na wenye uelewa wa washiriki na makundi katika hatua ya ufanyaji maamuzi husika.
4. Nchi zitafafanua, kutafsiri na kutumia mikataba na viwango husika vya

kimataifa ambayo wao ni washirika katika namna inayoakisi wajibu wao wa haki za kibinadamu kama zitumikavyo kwa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.

5. Nchi zitachukua hatua zote stahiki katika kuhakikisha wadau wasio wa kiserikali wako kwenye nafasi ya kuthibiti, mfano watu binafsi na mashirika, mashirika ya kimataifa na shughuli nyingine za kibiashara, kuheshimu na kuimarisha haki za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.
6. Nchi, kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa kwa kusaidia na jitihada za kitaifa katika kufikiwa kwa malengo na madhumuni ya Mkataba huu, zitachukua hatua stahiki na madhubuti katika suala hili, kati na baina ya nchi na, itakapofaa, kwa ubia na mashirika ya kimataifa na kikanda na asasi za kiraia, hususani mashirika ya wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini. Hatua hizo zinaweza kuhusisha:
  - a. Kuhakikisha kwamba mashirikiano ya kimataifa husika, ikiwamo programu za maendeleo za kimataifa, ni jumuisi, zinafikika na zina mahusiano na wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini;
  - b. Kuwezesha na kuchangia shughuli za kujenga uwezo, ikiwamo kubadilishana na kushirikishana taarifa, uzoefu, programu za mafunzo na mbinu bora;
  - c. Kuwezesha mashirikiano katika tafiti na upatikanaji wa maarifa ya kisayansi na kistadi;
  - d. Kutoa, itakapofaa, misaada ya kiuchumi na kistadi, kuwezesha upatikanaji na ushirikishwaji wa teknolojia rahisi, na kwa kuhamishiana teknolojia, hususani kwa nchi zinazoendelea, kwa makubaliano ya pande zote husika;
  - e. Kuboresha uendeshwaji wa masoko katika ngazi ya kidunia na kuwezesha upatikanaji wa taarifa za masoko kwa haraka, ikiwamo taarifa za akiba ya chakula, ili kusaidia kuepusha kukithiri kwa mfumuko ya bei ya chakula na mvuto wa uvumi.

### Ibara ya 3

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kufurahia kikamilifu haki zote za binadamu na misingi yote ya uhuru kama inavyotambulika katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Mkataba wa Haki za Binadamu na mikataba mingineyo ya kimataifa ya haki za binadamu, huru dhidi ya aina yeyote ya ubaguzi katika utekelezaji wa haki kwa misingi yeyote kama vile asili, utaiifa, rangi, uhamiaji, jinsi, lugha, utamaduni, hali ya ndoa, ulemavu, umri, siasa au mtazamo, dini au hadhi ya kuzaliwa au kiuchumi, kijamii au hadhi nyingine.
2. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kuchagua au kuunda vipaumbele na mikakati ya kutekeleza haki zao za maendeleo.

3. Nchi zitachukua hatua stahiki kuondokana na hali zitakazoweza kusababisha au kuchochea ubaguzi, ikiwamo aina mbalimbali ya ubaguzi wenyekuingiliana, dhidi ya wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.

#### **Ibara ya 4**

1. Nchi zitachukua hatua stahiki kuondokana na aina zote za ubaguzi dhidi ya wakulima wadogo wanawake na wanawake wengine wanaofanya kazi vijijini na kukuza uwezeshaji wao ili kuhakikisha, katika msingi wa usawa baina ya wanaume na wanawake, kwamba wanafurahia kikamilifu na kwa usawa haki zote za binadamu na misingi yote ya uhuru na wanaweza kusaka, kushiriki na kunufaika, kwa uhuru, maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kitamaduni vijijini.
2. Nchi zitahakikisha kwamba wakulima wadogo wanawake na wanawake wengine wanaofanya kazi vijijini wanafurahia haki zote za binadamu na misingi ya uhuru iliyoainishwa katika Mkataba huu na mikataba mengineyo yakimataifa ya haki za binadamu, kujumuisha haki:
  - a. Ya kushiriki kwa usawa na kikamilifu katika utunzi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika ngazi zote;
  - b. Ya upatikanaji kwa usawa viwango vya juu iwezekanavyo vya afya ya akili na kimwili, ikiwamo nyenzo za huduma toshelevu za afya, taarifa, ushauri na huduma katika uzazi wa mpango;
  - c. Ya kunufaika moja kwa moja kwa programu za kinga ya jamii;
  - d. Ya kupata mafunzo na elimu ya aina zote, rasmi au isiyo rasmi, ikiwamomafunzo na elimu inayohusiana na vitendo, na kunufaika na huduma zote za jamii na za ziada ili kukuza ufanisi wao kitaalam;
  - e. Ya kuanzisha vikundi vya kusaidiana, jumuiya na vyama vya ushirika ili kuweza kupata fursa za kiuchumi kwa usawa, kwa kuajiriwa au kujiajiri;
  - f. Ya kushiriki katika shughuli zote za jamii;
  - g. Ya kuzifikia huduma za kifedha, huduma ya kuweka na kukopa katika kilimo, huduma za masoko na teknolojia stahiki;
  - h. Ya upatikanaji sawa wa matumizi na usimamizi wa ardhi na rasilimali asili, na uhudumiaji sawa au wa kipaumbele katika mageuzi ya ardhi na katika mipango ya ugawaji ardhi;
  - i. Ya ajira zenye staha, malipo ya usawa na manufaa ya hifadhi ya jamii, na kuweza kuzifikia shughuli za uzalishaji mali;
  - j. Ya kuwa huru dhidi ya aina zote za ukatili.

#### **Ibara ya 5**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayo haki ya kuzifikia na kuzitumia, kwa namna endelevu, rasilimali asili zilizopo katika jamii zao zinazohitajika katika kuboresha hali zao za maisha, kwa mujibu wa



ibara ya 28 ya Mkataba huu. Pia wanayo haki ya kushiriki katika usimamizi wa rasilimali hizi.

2. Nchi zitachukua hatua kuhakikisha kwamba matumizi yeyote yale yanayoathiri rasilimali asili ambazo wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanazimiliki kimila au kutumia yanaruhusiwa kwa kuzingatia, bila ukomo wa:
  - a. Tathmini madhubuti iliyofanyika ya athari ya jamii na mazingira;
  - b. Ushirikishwaji kwa misingi wa nia njema, kwa mujibu wa ibara ya 2(3) ya Mkataba huu;
  - c. Mifumo ya haki na usawa katika kugawana faida ya uendelezaji uliokubalika katika makubaliano ya pande zote kati ya wanaotumia rasilimali asili na wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.

### **Ibara ya 6**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayo haki ya kuishi, utimamu wakimwili na kiakili, uhuru na ulinzi wa mtu.
2. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini hawatakuwa wahanga wa ukamataji holela na kuwekwa kizuizini, mateso au ukatili mwengine, udhalilishaji au matendo na adhabu zisizo za kiutu, na hawatashikiliwa kwa nguvu au kufanyawatumwa.

### **Ibara ya 7**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kutambulika mahali kote kama watu mbele ya sheria.
2. Nchi zitachukua hatua stahiki kuwezesha uhuru wa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini kwenda watakapo.
3. Nchi, zitakapohitajika, zitachukua hatua stahiki kushirikiana kushughulika na masuala ya umiliki yanayovuka mipaka ya kimataifa na kuwaathiri wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini, kwa mujibu wa ibara ya 28 ya Mkataba huu.

### **Ibara ya 8**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanaouhuru wa mawazo, imani, utambuzi, dini, maoni, kujieleza na kukusanyika kwa amani. Wanayohaki ya kueleza maoni, ama kwa sauti, kwa maandishi au katika machapisho, katika mfumo wa sanaa, au kwa njia nyingine wazipendazo, katika ngazi zote za kijamii, kitaifa, kikanda na kimataifa.
2. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya binafsi na/ au kwa pamoja, kwa kushirikiana na wengine au kama jamii,

kushiriki katika shughuli za amani za kupinga ukiukwaji wa haki za binadamu na misingi ya uhuru.

3. Utekelezaji wa haki husika katika ibara hii inabeba na wajibu na majukumu mahususi. Hivyo panaweza kuwa na mipaka, lakini hiyo sharti ielezwe bayana na sheria na ni muhimu:
  - a. Kwa kuheshimu haki au hadhi ya wengine;
  - b. Kwa ulinzi wa usalama wa taifa au kwa utulivu wa jamii au kwa afya ya jamii au maadili ya jamii.
4. Nchi zitachukua hatua zote stahiki kwa kutumia mamlaka zake madhubuti kuhakikisha ulinzi na usalama kwa wote, binafsi au kwa ujumla, dhidi ya vitisho, vurugu, visasi, ubaguzi wa kisheria na wa kimazingira, shinikizo au udhalimu wowote ule kama matokeo ya utekelezaji na ushiriki wake halali wa kutetea na kulinda haki zilizoelzwa katika Mkataba huu.

### **Ibara ya 9**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kuunda na kujiunga na mashirika, vyama vya wafanyakazi, ushirika au makundi au vyama vyovyote vingine watakavyohiyari kwa ajili ya ulinzi wa maslahi yao, ili kutetea matakwao yao. Vyombo hivyo vitakuwa huru na vya hiari, na vitabaki kuwa huru dhidi ya kuingiliwa, vitisho au ukandamizaji wa aina yeyote.
2. Hapatakuwa na mipaka itakayowekwa katika utekelezaji wa haki hii zaidi ya yale yaliyowekwa kwenye sheria na ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia katika maslahi ya usalama wa taifa, amani na usalama wa jamii, ulinzi wa afya au maadili ya jamii au katika ulinzi wa haki na uhuru wa watu wengine.
3. Nchi zitachukua hatua stahiki kuhamasisha uundwaji wa vyombo vya wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini, ikiwamo vyama, ushirika au mashirika mengine, hususani yenye mtizamo wa kuondokana na vikwazo katika uundwaji, ukuaji na uendeshaji wa shughuli zake halali, ikiwamo ubaguzi wa aina yeyote wa kisheria au kiutawala dhidi ya taasisi husika na wanachama wake, na kuwapatia msaada wa kuboresha nafasi na uwezo katika kupatana mipangilio ya mikataba ili kuhakikisha kwamba vigezo na bei zina tija na zilizohakika na zisizokiuka haki ya maisha ya staha na utu.

### **Ibara ya 10**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayo haki ya ushiriki hai na huru, moja kwa moja na/ au kwa kupitia vyombo vyao vya uwakilishi, katika maandalizi na utekelezaji wa sera, programu na miradi inayoweza kuathiri maisha, ardhi na ustawi wao.
2. Nchi zitahamasisha ushiriki, wa moja kwa moja na/ au kupitia vyombo vyao vya uwakilishi, wa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi

vijijini katika michakato ya ufanyaji maamuzi yanayoweza kuathiri maisha, ardhi na ustawi wao; hii ni pamoja na kuheshimu uanzishwaji na ukuaji wa vyombo imara na huru vya wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini na kuhamasisha ushiriki wao katika maandalizi na utekelezaji wa viwango vya uthibiti vya usalama wa chakula, kazi na mazingira vinavyoweza kuwaathiri.

### **Ibara ya 11**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kusaka, kupokea, kuzalisha na kuwasilisha taarifa, ikiwamo taarifa ya masuala yanayoweza kuathiri uzalishaji, uchakataji, uuzaji na usambazaji wa mazao yao.
2. Nchi zitachukua hatua stahiki katika kuhakikisha wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanaouwezo wa kupata taarifa zinazowahusu, kwa uwazi, kwa wakati na zinazojitoshelezakatika lugha na mtindo na kwa namna inayoakisi njia ya tamaduni zao ili kukuza uwezo wao na kuhakikisha ushiriki wao kikamilifu katika ufanyaji maamuzi ya masuala yanayoweza kuathiri maisha, ardhi na ustawi wao.
3. Nchi zitachukua hatua stahiki za kukuza ufikiwaji wa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini na mifumo sahihi, rafiki na huru ya uthaminishaji na uidhinishaji viwango vya ubora vya mazao na bidhaa zao katika ngazi ya msingi, kitaifa na kimataifa, na kuhamasisha ushiriki wao katika uundaji wake.

### **Ibara ya 12**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kupata haki madhubuti na bila ubaguzi, ikiwamo kufuatwa taratibu za haki katika usuluhishi wa migogoro na upatiwaji wa stahiki kikamilifu kwa ukiukwaji wa haki zao za kibinadamu. Maamuzi hayo yatazingatia tamaduni, mila, taratibu na sheria zao kwa kuzingatia wajibu husika katika sheria za haki za binadamu za kimataifa.
2. Nchi, kupitia vyombo adilifu na madhubuti vya mahakama na utawala, zitatoa nafasi zisizo za kibaguzi, rafiki na madhubuti za usuluhishi kwa wakati katika lugha ya wahusika, na zitatoa stahiki kamilifu na ndani ya muda, ambazo zinaweza kujumuisha haki ya kukata rufaa, kulipwa fidia, kurejeshewa gharama, kufidiwa hasara na kufanyiwa matengenezo.
3. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kupata usaidizi wa kisheria. Nchi zitazingatia njia za ziada, ikiwamo utoaji msaada wa kisheria, kusaidia wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini ambao vinginevyo hawataweza kuvifikia vyombo vya kiutawala na mahakama.
4. Nchi zitazingatia hatua za kuboresha vyombo husika vya kitaifa vya

kuhamasisha na kusimamia haki za binadamu, ikiwamo haki zinazoelezwa katika Mkataba huu.

5. Nchi zitawapatia Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini mfumo thabiti wa kudhibiti na kushughulika na masuala yanayolenga au kupelekea kukiukwa kwa haki za binadamu, unyanyanyi holela wa ardhi na rasilimali asili zao au kuwapoka utu au njia zao za kujikimu, na kwa mfumo wowote ule wa shuruti wa kuwaweka pamoja au kuhamisha.

### Ibara ya 13

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kufanya kazi, ikiwamo haki ya kuchagua namna yao kujipatia kipato.
2. Watoto wa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kulindwa dhidi ya kazi yeyote ile inayoweza kumuathiri au kumingilia kielimu, au yenye madhara kwa afya au maendeleo yake ya akili, mwili, roho, maadili na kijamii.
3. Nchi zitatengeneza mazingira rafiki na wezeshi yenye fursa za kazi kwa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini na familia zao zitakazo toa kipato kuwawezesha kuishi maisha ya staha.
4. Katika nchi zinazokabiliwa na viwango vya juu vya umaskini vijijini na kwa ukosefu wa fursa za ajira katika sekta nyingine, nchi zitachukua hatua stahiki katika kuanzisha na kuhamasisha mifumo endelevu ya chakula ambayo ni toshelevu kwa matumizi ya nguvu kazi itakayoweza kuchangia katika kuunda ajira nzuri.
5. Nchi, kwa kuzingatia tabia za kilimo kidogo na uvuvi mdogo, zitasimamia uzingatiaji wa sheria za kazi kwa kuweka, itakapohitajika, rasilimali stahiki kuhakikisha utendaji madhubuti wa ukaguzi wafanyakazi vijijini.
6. Hakuna mtu yeyote atakayehitajika kufanyakazi kwa lazima, kulazimishwa au kushurutishwa, atakayewekwa katika hatari itakayompelekea kuwa muathirika wa biashara ya usafirishaji haramu wa watu au atakayeshikiliwa kwa namna yeyote ya utumwa wa leo. Nchi, kwa kushauriana na kushirikiana na wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini na taasisi zao husika, zitachukua hatua stahiki kuhakikisha ulinzi dhidi ya unyonyaji wa kiuchumi, ajira kwa mtoto na aina zote za utumwa wa kileo, kama wanawake, wanaume na watoto kufanywa mateka wa mikopo, na ajira za lazima, ikiwamo za wavuvi na wafanyakazi katika uvuvi, wafanyakazi wa misituni au wafanyakazi wa msimu au wahamiaji.

### Ibara ya 14

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini, bila kujali ni wafanyakazi wa muda, msimu au wahamiaji, wanayohaki ya kufanya kazi katika mazingira safi na salama, kushiriki katika matumizi na mapitio ya hatua zakiusalama na kiafya, kuchagua wawakilishi wa

usalama na afya katika kamati za usalama na afya, katika utekelezaji wa hatua za kuzuia, kupunguza na kudhibiti hatari na athari, kuweza kupata mavazi na zana toshelevu na shatiki za kujikinga na taarifa na mafunzo sahihi kuhusu ulinzi kazini, kufanya kazi kwa uhuru bila unyanyasaji na ukatili, ukiwamo unyanyasaji wa kingono, kutoa taarifa mazingira mabovu na hatarishi ya kazi na kujinusuru na hatari itokanayo na kazi pale ambapo wanapojidhihirisha kwamba kuna hatari kwa afya na usalama wao, pasipo kuwa na kisasi chochote cha kazi kitakachotokana na wao kutekeleza haki zao.

2. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kutokutumia na kujihatarisha na zana hatari na kemikali zenye sumu, kujumuisha kemikali za kilimo au vichafuzi katika kilimo au viwandani
3. Nchi zitachukua hatua stahiki kuhakikisha mazingira rafiki na salama ya kazi kwa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini, na zitaweka hususani mamlaka madhubuti zinazohusika na zitaweka mifumo ya uratibu baina ya sektakwa ajili ya utekelezaji wa sera na usimamizi wa sheria za nchi na kanuni za usalama na afya kazini katika kilimo, viwanda vya kilimo na uvuvi, kuelekeza kwa hatua za marekebisha na adhabu, na kuweka na kusaidia mifumo stahiki ya uangalizi wa maeneo ya kazi vijijini.
4. Nchi zitachukua hatua zote stahiki kuhakikisha:
  - a. Kujikinga na athari za kiafya na kiusalama zinazotokana na teknolojia, kemikali na shughuli za kilimo, ikiwamo kwa kuzikataza au kuzizuia;
  - b. Kuidhinishwa, na mamlaka husika, mfumo stahiki wa kitaifa au mfumo mwingine wowote unaoanzisha masharti mahususi ya uingizaji, utengaji, ufungaji, usambazaji, utambulishaji na matumizi ya kemikali zinazotumika katika kilimo, na kwa ajili ya kuyazuia au kuyakataza;
  - c. Kuwa wote wanaohusika na kuzalisha, kuingiza, kutoa, kuza, kusambaza, kutunza na kuharibu kemikali zinazotumika katika kilimo wanazingatia kanuni na viwango vya usalama na afya vya nchi au vinginevyo, na wanatoa taarifa stahiki na zinazojitosheleza kwa watumiaji katika lugha rasm au lugha za nchi na, kwa maombi, kwa mamlaka husika;
  - d. Kuna mfumo unaofaa na salama wa kukusanya, kuchakata na kuharibu kemikali chafu, kemikali isiyofaa kwa matumizi na makontena ya kemikali ili kuepusha matumizi yake kwa madhumuni mengine na kuondokana au kupunguza hatari za kiusalama, afya na mazingira;
  - e. Uandaaji na utekelezaji wa programu za elimu na kukuza uelewa kwa jamii juu ya athari za kiafya, usalama na mazingira kwa kemikali zinazotumika mara nyingi vijijini, na kuhusiana na mibadala yake.

## Ibara ya 15

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya chakula cha kujitosheleza na haki ya msingi ya kuwa huru dhidi ya njaa.

- Hii inajumuisha haki ya kuzalisha chakula na haki ya lishe inayojitosheleza, inayowahakikisha uwezekano wa kufurahia viwango vya juu vya maendeleo ya mwili, hisia na akili.
2. Nchi zitahakikisha kwamba wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanafurahia kwa muda wote upatikanaji wa kiumbo na kiuchumi wa chakula kinachojitosheleza na kinachozalishwa na kinacholiwa kiuendeleu na kiusawa, kwa kuheshimu tamaduni zao, kwa kutunza upatikanaji wa chakula kwa vizazi vijavyo, na kinacho wahakikishia kujitosheleza kimwili na kiakili na maisha ya staha kwao, binafsi na/au kwa pamoja kuzingatia mahitaji yao.
  3. Nchi zitachukua hatua stahiki kukabiliana na ukosefu wa lishe vijijini, ikiwamondani ya mfumo wa huduma ya msingi ya afya kupitia, miongoni mwa mengine, matumizi ya teknolojia iliyopo na utoaji wa vyakula lishe vingine toshelevu na kuhakikisha wanawake wanalithe wakati wa ujauzito na kipindi cha kunyonyesha. Nchi zitahakikisha kuwa makundi yote ya kijamii, hususani wazazi na watoto, wanataarifa, wanafikia elimu ya lishe na wanasaidiwa katika matumizi ya maarifa ya msingi kuhusu lishe ya motto na faida ya kunyonyesha.
  4. Wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kuchagua mifumo yao ya chakula na kilimo, kama inavyotambulika katika nchi nyingi na kanda kama uhuru wa chakula. Hii inajumuisha haki ya kushiriki katika mchakato kufanya maamuzi katika sera ya chakula na kilimo na haki ya afya njema na uzalishaji chakula unaojitosheleza kwa njia makini za kiikolojia na mbinu endelevu zinazoheshimu tamaduni zao.
  5. Nchi zitaunda, kwa mashirikiano na wakulima na watu wanaofanyakazi vijijini, sera za umma katika ngazi za jamii, taifa, kanda na kimataifa kwa ajili ya kuendeleza na kulinda haki ya kujitosheleza kwa chakula, uhakika wa chakula na uhuru wa chakula na mifumo ya chakula iliyoendeleu na yenye usawa inayoeneza na kulinda haki zilizomo katika Mkataba huu. Nchi zitaanzisha mifumo itakayohakikisha kushaabianakwa sera zake za kilimo, uchumi, kijamii, kiutamaduni na maendeleo na utekelezaji wa haki zilizomo kwenye Mkataba huu.

## Ibara ya 16

1. Wakulima na watu wanaofanya kazi vijijini wanayo haki ya kuishi maisha ya staha wao wenyewe na familia zao kuwezesha kupata nyenzo muhimu za uzalishaji zitakazowasaidia kuyafikia maisha hayo, ikiwamo zana za uzalishaji, msaada wa kitaaluma na vifaa, mikopo, bima na huduma nyengine za kifedha. Pia wanayo haki ya kushiriki kwa uhuru, kibinafsi na/au kwa makundi, kwa kujumuika na wengine au kama jamii, katika njia za asili za kilimo, uvuvi, ufugaji na shughuli za misituni na kuunda mifumo ya biashara ya kijamii.
2. Nchi zitachukua hatua stahiki za upendeleo kuwezesha wakulima na watu wanaofanya kazi vijijini kuzifikia njia za usafirishaji na uchakatishaji,

vifaa vya ukaushaji na uhifadhi vilivyo vya lazima kwaajili ya kuuza mazao yao katika masoko ya jamii zao, nchi na ya ukanda wao kwa bei zitakazowawezesha wao na familia zao kupata pato la haki kuishi maisha ya staha.

3. Nchi zitachukua hatua stahiki kuimarisha na kusaidia masoko ya kijamii, kitaifa na kikanda katika namna zinazowezesha na kuhakikisha wakulima na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanauwezo sawa na kamili wa kufikia na kushiriki katika masoko kuuza bidhaa zao katika bei zitakazowawesha wao na familia zao kuweza kuishi maisha ya staha.
4. Nchi zitachukua hatua zote stahiki kuhakikisha sera na programu zao za maendeleo vijijini, kilimo, mazingira, biashara na uwekezaji zinachangia kikamilifu kulinda na kuimarisha hali za maisha vijijini na mabadiliko ya kuelekea katika aina ya uzalishaji endelevu katika kilimo. Nchi zitahamasisha uzalishaji endelevu, kujumuisha kilimo cha kiikolojia na uzalishaji wa kiogani, pale inapowezekana, na zitawezesha mauzo ya moja kwa moja kati ya mkulima na mlaji.
5. Nchi zitachukua hatua stahiki kuimarisha uwezo wa wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini kukabiliana na majanga ya asili na changamoto nyingine, kama kudhorota kwa soko.
6. Nchi zitachukua hatua stahiki kuhakikisha malipo ya staha na yenye usawa kwa kazi zenye thamani sawa, pasipo utofauti wa aina yeyote.

## Ibara ya 17

1. Wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini wanayohaki, binafsi na/ au kwa pamoja, katika ardhi kwa mujibu wa ibara ya 28 ya Mkataba huu, ikiwamo haki ya kupata, kutumia kiuendelevu na kusimamia ardhi na vyanzo vya maji, uvuvi, mifugo na misitu iliyopo, kuyafikia maisha ya kujitoshesha, kuweza kuishi maisha yenye usalama, amani na staha na yenye kuendeleza tamaduni zao.
2. Nchi zitachukua hatua stahiki kuondoa na kudhibiti hali zote za ubaguzi kuhusiana na haki za ardhi, zikiwemo zile zinazotokana na kubadilika kwa hali ya kindoa, ukosefu wa hadhi ya kisheria au kushindwa kuzifikia rasilimali za kiuchumi.
3. Nchi zitachukua hatua stahiki kutambua haki za umiliki wa ardhi kisheria, kujumuisha haki za umiliki wa kimila ambao hautambuliki hivi sasa kisheria, kwa kutambua uwepo wa mifumo na miundo tofauti. Nchi zitalinda umiliki halali wa ardhi na zitahakikisha wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini hawaondolewi kiholela wala kwa kutofuata sheria na kwamba haki zao hazita vinginevyo kiukwa au kupuuzwa. Nchi zitatambua na kulinda maeneo asili ya jumuiia na kutambua mfumo wa pamoja wa matumizi na usimamizi wa maeneo hayo.
4. Wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kulindwa dhidi ya uhamishwaji holela au unaokiuka sheria kutoka kwenye ardhi au maeneo yao ya makazi, au kutoka kwenye maliasili nyenginezo ambazo

hutumika katika shughuli zao na muhimu kwao kwa ajili ya kufurahia maisha ya staha. Nchi zitajumuisha ulinzi dhidi ya uhamishaji katika sheria za ndani zinazoakisi sheria za kimataifa za kibinadamu na haki za binadamu. Nchi zitakataza ufukuzaji/ uondoshaji holela na usiozingatia sheria na wa nguvu, uharibifu wa maeneo ya kilimo na uporaji au unyang'anyi wa ardhi na maliasili nyinginezo, ikiwamo kama hatua za adhabu au nyenzo au mbinu ya vita.

5. Wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini ambao wameondolewa kiholela au kwa njia zilizokuwa sheria na kunyimwa haki zao katika ardhi, binafsi au kwa pamoja, kwa kushirikiana na wengine au kama jamii, wanayohaki ya kurudi katika ardhi yao ambayo wamenyang'anywa kiholela na pasipo kufuata sheria, ikiwamo na wale waliokumbwa na majanga asili au/na migogoro ya kivita nao wanapaswa kurejeshewa haki yao ya kuzifikia na kuzitumia maliasili walizokuwa wakizitumia katika shughuli zao na muhimu kwaajili ya kufurahi mazingira bora ya kuishi, inapowezekana, au kupata fidia ya haki, stahiki na halali pale itakaposhindikana kurejea katika maeneo yao.
6. Inapobidi, nchi zitachukua hatua stahiki katika kufanikisha mageuzi ya kilimo ili kuwezesha upatikanaji, ulio mpana na wenye kuzingatia usawa, wa ardhi na rasilimaliasili nyinginezo zilizo muhimu katika kuhakikisha wakulima na watu wanaofanya kazi vijijini wanafurahia mazingira mazuri ya kuishi, na kuzuia ulindikizwaji na udhibiti uliokithiri katika ardhi, ukizingatia matumizi yake ya kijamii. Wakulima wadogo wasio na ardhi, vijana, wavuvi wadogo na wafanyakazi wengine vijijini wanapaswa kupewa kipaumbele katika ugawiwaji wa ardhi ya jumla, ya uvuvi na hifadhi.
7. Nchi zitachukua hatua stahiki zinazoelekezwa katika uhifadhi na matumizi endelevu ya ardhi na rasilimaliasili nyenginezo zinazotumika katika uzalishaji, ikiwamo kupitia kilimo cha kiikolojia, na kuhakikisha mazingira ya uendelevu katika uzalishaji wa kibaiolojia na wa mifumo mengine ya kiasili.

## Ibara ya 18

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki katika uhifadhi na ulinzi wa mazingira na kuwa na uwezo wa uzalishaji katika ardhi yao, na wa malighafi wanazozitumia na kuzisimamia.
2. Nchi zitachukua hatua stahiki kuhakikisha wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanafurahia, pasipo kubaguliwa, mazingira yaliyo safi na salama.
3. Nchi zitazingatia wajibu wao husika wa kimataifa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki katika kuchangia katika uundaji na utekelezaji wa sera za kijamii na kitaifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, ikiwamo kupitia matumizi ya taratibu na ujuzi wa asili.
4. Nchi zitachukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba hakuna vitu vya



hatari, uchafu au taka vinahifadhiwa au kutupwa katika ardhi ya wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini, na zitashiriki katika kukabiliana na hatari zozote za kimazingira zitakazowaathiri katika kufurahia haki zao.

5. Nchi zitawalinda wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini dhidi ya ukandamizaji watu au makundi yasiyo wa kiserikali, ikiwamo kwa kusimamia sheria za kimazingira zinazochangia moja kwa moja katika ulinzi wa haki za wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini.

## Ibara ya 19

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki katika mbegu, kwa mujibu wa Ibara ya 28 ya Mkataba huu, ikiwamo:
  - a. Haki ya ulinzi wa ujuzi wa asili kuhusiana na rasilimali jeni za mimea ya chakula na kilimo;
  - b. Haki ya kushiriki kwa usawa katika kushirikishana manufaa yatokanayo na matumizi ya rasilimali jeni za mimea ya chakula na kilimo;
  - c. Haki ya kushiriki katika kufanya maamuzi kuhusiana na masuala yanayohusiana na uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali jeni za mimea ya chakula na kilimo;
  - d. Haki ya kuhifadhi, kutunza, kutumia, kubadilishana na kuuza mbegu zao za shamba walizozitunza au vipandikizi.
2. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kuendeleza, kudhibiti, kulinda na kuzalisha mbegu zao na ujuzi wao wa asili.
3. Nchi zitachukua hatua kuheshimu, kulinda na kukamilisha haki za mbegu kwa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.
4. Nchi zitahakikisha kwamba mbegu za ubora na kiwango cha kujitosheleza zinapatikana katika kipindi bora cha kupanda na katika gharama nafuu.
5. Nchi zitatambua haki za wakulima wadogo kutegemea mbegu zao au mbegu za chaguo lao zinazopatikana katika jamii zao na kuamua wenyewe juu ya mazao wanayotaka kupanda.
6. Nchi zitachukua hatua stahiki kusaidia mifumo ya mbegu ya wakulima wadogo na kuhamasisha matumizi ya mbegu zao na kilimo cha bio-anuwai.
7. Nchi zitachukua hatua stahiki kuhakikisha tafiti na maendeleo katika kilimo zinajumuisha mahitaji ya wakulima wadogo na watu wanaofanya kazi vijijini, ilikuhakikisha ushiriki wao katika kutambua vipaumbele na shughuli za utafiti na maendeleo, kwa kuzingatia uzoefu wao, na kuongeza uwekezaji katika tafiti na uendelezaji wa mbegu na mazao kiwa yanayokidhi mahitaji ya wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.
8. Nchi zitahakikisha kwamba sera za mbegu, ulinzi wa mimea anuwai na sheria nyengine za hatimiliki, skimu za utoaji vyeti na sheria za uuzaji wa mbegu zinaheshimu na kuzingatia haki, mahitaji na uhalisia wa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.

## Ibara ya 20

1. Nchi zitachukua hatua stahiki, kwa mujibu wa wajibu wao husika wa kimataifa, kudhibiti uharibifu na kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya bioanuwai ili kuhamasisha na kulinda upatikanaji kamili wa haki za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.
2. Nchi zitachukua hatua stahiki kuhamasisha na kulinda ujuzi wa asili, ubunifu na utendaji wa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini, ikiwamo kilimo cha asili, ufugaji, uvuvi, mifumo ya kilimo cha kiikolojia na ufugaji ambayo inahusiana na uhifadhi na matumizi endelevu ya viumbe hai anuwai.
3. Nchi zitaepusha hatari ya ukiukwaji wa haki za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini zitokanazo na uendelezaji, uhifadhi, usafirishaji, matumizi, uhamishaji au utolewaji wa viumbe hai vilivyoboreshwa.

## Ibara ya 21

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanazohaki za binadamu za maji safi na salama ya kunywa na kutumia, ambayo ni muhimu kwa ajili ya kufurahia kikamilifu maisha, haki zote za binadamu na utu. Haki hizi hujumuisha mifumo bora ya usambazaji wa maji na vifaa vyake vilivyo katika hali bora, inayofikika na isiyo ya kibaguzi na yenye kukubalika katika misingi ya kijinsia na kitamaduni.
2. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki katika maji kwa ajili ya matumizi binafsi na nyumbani, kilimo, uvuvi na ufugaji na kwa kuhakikisha matumizi mengine ya kimaisha yahasuyo matumizi ya maji, kuhakikisha uhifadhi, uboreshaji na matumizi endelevu ya maji. Wanayohaki ya upatikanaji sawa wa maji na mifumo ya upatikanaji maji na wawe huru dhidi ya ukatiwaji holela au uchafuzi wa vyanzo vya maji.
3. Nchi zitaheshimu, kulinda na kuhakikisha upatikanaji wa maji, ikiwamo katika mifumo ya asili na kijamii ya uratibu mifumo maji, isiyo katika misingi ya kibaguzi, na zitachukua hatua kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi binafsi, matumizi ya ndani na matumizi ya uzalishaji, na kuboresha usafi, hususani kwa ajili ya wanawake na wasichana waishio vijijini na watu waliokatika mazingira magumu na makundi ya pembezoni, kama wafugaji wanaohama hama, wafanyakazi wa mashamba makubwa, wahamiaji wote pasipo kujali hadhi yao na watu wanaoishi katika makazi yasiyorasmi na ambayo hayajapangiliwa. Nchi zitahamasisha teknolojia rafiki, ikiwemo teknolojia ya umwagiliaji, ya kutibu majitaka kwaajili ya matumizi tena, na ya ukusanyaji na uhifadhi maji.
4. Nchi zitatumiza na kurejesha mifumo ya vyanzo vya maji vya asili, ikiwemo milima, misitu, chemchem, maeneo oevu, mito na maziwa, dhidi ya matumizi yanayozidi uwezo na kuharibiwa kwa matumizi ya zana hatarishi, hususani

zitokanazo na madini na kemikali za viwandani yatakayoweza kupelekea uharibifu wa haraka au taratibu kwa usumu husika.

5. Nchi zitadhibiti watu/ makundi mengine yasadumaze haki ya kufurahia maji kwa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini. Nchi zitatoa kipaumbele cha maji katika mahitaji ya kibinadamu kabla ya mahitaji mengine, ikihamasisha uhifadhi, udhibiti na matumizi endelevu.

## Ibara ya 22

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayo haki ya hifadhi jamii ikiwamo bima jamii.
2. Nchi, kwa kulingania muktadha wake, zitachukua hatua stahiki kuhamasisha ufurahiaji wa haki ya hifadhi jamii kwa wafanyakazi wahamiaji wa maeneo ya vijijini.
3. Nchi zitatambua haki za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini katika hifadhi jamii, kujumuisha bima jamii, na kwa mujibu wa muktadha wake, zitaanzisha au kuendeleza mifumo yake ya kinga jamii inayojumuisha manufaa ya msingi ya hifadhi jamii. Yakuhakikishwa yanapaswa kwa kiwango cha chini kuwa, katika mzunguko wa maisha, watu wote wenye uhitaji wanaweza kuzifikia huduma muhimu za afya na kupata ulinzi wa kipato cha msingi, ambayo kwa pamoja yatahakikisha upatikanaji makini wa mali na huduma zinazotambulika kuwa muhimu nchini.
4. Mahitaji ya msingi ya hifadhi jamii yanapaswa kuwekwa na sheria. Taratibu za malalamiko na rufaa, zilizo huru, wazi, rafiki na makini zinapaswa kuelezwa. Mifumo inabidi iwekwe kuhakikisha kuzingatiwa kwa mifumo ya kisheria ya nchi.

## Ibara ya 23

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kufarahia kiwango cha juu kabisa kiwezekanacho cha afya ya mwili na akili. Pia wanayohaki ya kuzifikia huduma zote za kijamii na afya, pasipo aina yoyote ya ubaguzi.
2. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kutumia na kuzilinda tiba zao za asili na kuendeleza taratibu zao za afya, ikiwamo haki yao ya kuifikia na kuhifadhi mimea, wanyama na madini kwaajili ya dawa.
3. Nchi zitahakikisha upatikanaji wa huduma, vifaa na amali za afya vijijini katika misingi isiyo ya kibaguzi, hususani kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi; upatikanaji wa dawa, chanjo dhidi ya magonjwa makuu ya kuambukiza, afya ya uzazi, taarifa kuhusiana na masuala ya misingi ya kiafya yanayoathiri jamii, kujumuisha njia za kujikinga na kujidhibiti, huduma ya afya ya mama na mtoto, pamoja na mafunzo ya watumishi wa afya, ikiwamo elimu ya haki za afya na binadamu.

**Ibara ya 24**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya makazi bora. Wanayohaki ya kupata nyumba na jamii za kuishi kwa amani na staha, na haki ya kutobaguliwa katika muktadha huo.
2. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kulindwa dhidi ya kufukuzwa kwa nguvu, manyanyaso na vitisho katika makazi yao.
3. Nchi hazitawaondoa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini kinyume cha hiari yao, kiholela au pasipo kuzingatia sheria, ama kwa muda au moja kwa moja, kwenye makazi au ardhi yao wanayoishi pasipo kuwapatia au kuwahakikishia ulinzi stahiki wa kisheria na ulinzi mwengine. Endapo uhamishaji ni wa lazima, nchi lazima zitoe au zihakikishe utoaji wa fidia ya haki na sawa kwa upotevu wa mali na mwengine wowote.

**Ibara ya 25**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya mafunzo ya kutosheleza yanayokidhi mahususi kilimo cha kiikolojia, utamaduni jamii na mazingira ya kiuchumi ambayo wanaishi. Masuala yaliyomo katika programu za mafunzo yajumuishe, lakini yasiishie kwenye, kukuza uzalishaji, uuzaji na uwezo wa kukabiliana na wadudu waharibifu, wanyama, mitikisiko ya kimfumo, athari ya kemikali, mabadiliko ya tabia nchi na matukio ya hali ya hewa.
2. Watoto wote wa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya elimu kwa mujibu wa utamaduni wao na wa haki zote zinazoeleza na sheria za haki za binadamu.
3. Nchi zitahimiza ubia wenye usawa na shirikishibaina ya wanasayansi na wakulima, kama shule za vitendo za kilimo, uchavushaji shirikishi wa mazao na kliniki za afya ya mimea na wanyama, kushughulikia changamoto za wakati husika na zinazojitokeza na zinazowakabili wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.
4. Nchi zitawekeza katika kutoa mafunzo, taarifa za masoko na huduma ya ushauri katika ngazi ya mashambani.

**Ibara ya 26**

1. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki ya kufurahia utamaduni wao na kushiriki kwa uhuru katika maendeleo ya tamaduni zao, pasipo kuingiliwa au aina yoyote ya ubaguzi. Pia wanayohaki ya kuendeleza, kueleza, kudhibiti, kulinda na kuzalisha ujuzi wao asili na kijamii, kama namna wanavyoishi, njia za uzalishaji au teknolojia, au mila na desturi.  
Hakuna mtu anayeweza kuhalalisha haki za kiutamaduni zinazokiuka au

- kudhibiti haki za binadamu zinazoelezwa na kuhakikishwa na sheria za kimataifa.
2. Wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini wanayohaki, binafsi na/au kama kundi, kwa kushirikiana na wengine au kama jamii, kueleza mila za jamii zao, lugha, tamaduni, imani, fasihi na sanaa zao, kwa kuzingatia na viwango vya haki za kibinadamu za kimataifa.
  3. Nchi zitaheshimu na zitachukua hatua kutambua na kulinda, haki za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini zinazohusiana na ujuzi wao wa asili, na kuondokana na ubaguzi dhidi ya ujuzi wa asili, shughuli/taratibu na teknolojia za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini.


### **Ibara ya 27**

1. Wakala maalum, mifuko na programu za Umoja wa Mataifa na za mashirika mengine ya kimataifa, ikiwamo mashirika ya kimataifa na kikanda ya fedha, yatachangia katika ufanikishaji wa Mkataba huu, ikiwamo katika utafutaji, miongoni mwa mambo mengine, wa misaada ya maendeleo na mashirikiano. Njia na namna ya kuhakikisha ushiriki wa wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini katika masuala yanayowaathiri yatazingatiwa.
2. Umoja wa Mataifa na wakala zake maalum, mifuko na programu, na mashirika mengine ya kimataifa, ikiwamo mashirika ya kimataifa na kikanda ya fedha, yatahamasisha uzingatiaji wa utekelezaji kamili wa Mkutano huu na kufuatilia katika ufanisi wake.

### **Ibara ya 28**

1. Hakuna jambo katika Azimio hili linaweza kuchukuliwa kama linakandamiza, kupuuza au kuathiri haki za wakulima wadogo na watu wengine wanaofanya kazi vijijini na wakaazi wenyeji ambazo wanazo hivi sasa au watakazo kuwa nazo siku zijazo.
2. Haki za binadamu na misingi ya haki kwa wote, pasipo ubaguzi wa aina yeyote, zitaheshimiwa katika utekelezaji wa haki zinazoelezwa na Mkataba huu. Utekelezaji wa haki zilizozezwa katika Mkataba huu utakuwa na udhibiti pekee utakaotambuliwa kisheria na utakaozingatia wajibu wa kimataifa wa haki za binadamu. Udhibiti wa aina hii hautakuwa wa kibaguzi na utakuwa wa muhimu tu katika kuhakikisha utambuzi na uzingativu wa haki na uhuru wa wengine na katika kukidhi hitaji la misingi la haki katika jamii ya kidemokrasia.

# KURA ZA MKUTANO MKUU WA UM KUHUSIANA NA MKATABA WA UMOJA WAKULIMA WADOGO NA WATU WENGINE WANAOFAM




- 10 Zisizopiga Kura
- 8 Kura za Hapana
- 54 Ambao hawakupiga Kura
- 121 Kura za Ndio

**VOTE FINAL :**

Mipaka na majina yaliyomo na maeneo yaliyotumika katika ramani hii hayaelezi maoni yeyote yale ya upande wa La Via Campesina kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yeyote, sehemu, mji au eneo lolote au mamlaka yake, au kuhusiana na uwekaji wa mipaka

54  
10

# OJA WA MATAIFA WA MATAIFA WA NYA KAZI VIJIJINI



121 IN FAVOUR

4 ABSTAINING  
NON-VOTING

## Nchi zilizopiga kura ya ndio

Afghanistan, Algeria, Angola, Antigua na Barbuda, Azerbaijan, Bahamas, Bahran, Bangladesh, Barbados, Belarus, Belize, Benin, Bhutan, Bolivia, Botswana, Brunei Darussalaam, Burundi, Cape Verde, Cambodia, Jamhuri ya Kati, Chad, Chile, China, Comoros, Costa Rica, Cuba, Ivory Coast, Jamhuri ya Watu wa Korea, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Djibouti, Domicia, Jamhuri ya Dominica, Ecuador, Misri, El Salvador, Eritrea, Gabon, Gambia, Ghana, Grenada, Guinea, Guinea-Bissau, Guyana, Haiti, India, Indonesia, Iran (Jamhuri ya Kiislam ya), Iraq, Jamaica, Jordan, Kazakhstan, Kenya, Kuwait, Kyrgyzstan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao, Lebanoni, Libya, Luxemborg, Madagascar, Malawi, Malaysia, Maldives, Mali, Mauritania, Mauritius, Mexico, Monaco, Mongolia, Morocco, Mozambique, Myanmar, Namibia, Nepal, Nicaragua, Niger, Nigeria, Oman, Pakistan, Panama, Papua New Guinea, Peru, Ufilipino, Ureno, Qatar, Jamhuri ya Moldova, Rwanda, Saint Kitts and Nevis, Saint Lucia, Saint Vicent na Grenadines, Sao Tome na Principle, Saudia Arabia, Senegal, Serbia, Afrika ya Kusini, Sri Lanka, Sudan, Sudan ya Kusini, Suriname, Uswizi, Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, Tajikistan, Thailand, Timor-Leste, Togo, Trinidad na Tobago, Tunisia, Uganda, Falme za Kiarabu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Uruguay, Uzbekistan, Venezuela (Jamhuri ya Bolivaria ya), Vietnam, Yemenni, Zambia, Zimbabwe

## Nchi zilizopiga kura ya hapa

Australia, Guetamala, Hungary, Israel, New Zealand, Sweden, Uingereza na Ireland Kaskazini, Marekani

## Nchi ambazo hazikupiga kura

Albania, Andorra, Argentina, Armenia, Austria, Ubelgiji, Bosnia na Herzegovina, Brazil, Bulgaria, Cameroon, Canada, Colombia, Croatia, Cyprus, Jamhuri ya Czech, Denmark, Estonia, Ethiopia, Fiji, Finland, Ufaransa, Georgia, Ujerumani, Ugiriki, Honduras, Iceland, Irelad, Italia, Japan, Kiribati, Latviam, Lesotho, Liechtenstein, Lithuania, Malta, Montenegro, Netherlands, Norway, Palau, Poland, Jamhuri ya Korea, Romania, Urusi, Samoa, San Marino, Singapore, Slovakia, Slovenia, Hispania, Jamhuri ya zamani ya Yugoslav ya Macedonia, Uturuki, Tuvalu, Ukraine, Vanuatu

## Nchi ambazo hazipigi kura

Turkmenistan, Eswatini, Burkina Faso, China, Jamhuri ya Nauru, Micronesia, Marshall Islands, Tonga, Paraguay, Equatorial Guinea.













**La Via Campesina**  
**International Secretariat**  
**Stand No. 197A, Smuts Road Prospect**  
**Waterfalls – Harare – Zimbabwe**  
**viacampesina@viacampesina.org**

**[www.viacampesina.org/en](http://www.viacampesina.org/en)**  
**[tv.viacampesina.org](http://tv.viacampesina.org)**

** ViaCampesinaOfficial  @via\_campesina**